Madarasa ya miaka tofauti: karatasi ya ukweli kwa wazazi na walezi

Je, madarasa ya miaka tofauti ni nini?

Madarasa ya miaka tofauti yanajumuisha wanafunzi kutoka ngazi ya zaidi ya mwaka mmoja. Madarasa haya yanaweza kujumuisha wanafunzi katika hatua moja ya mtaala au kutoka hatua nyingi za mtaala.

Mtaala wa NSW umepangwa katika hatua hizo zifuatazo:

Hatua ya Mapema ya 1: Chekechea

Hatua ya 1: Mwaka wa 1 na Mwaka wa 2

Hatua ya 2: Mwaka wa 3 na Mwaka wa 4

Hatua ya 3: Mwaka wa 5 na Mwaka wa 6

Wanafunzi hujifunza kutoka hatua ile ya mtaala inayohusika kwao, kama wapo katika darasa la miaka tofauti au la mwaka mmoja. Kwa mfano, mwanafunzi wa Mwaka wa 2 katika darasa la Mwaka wa 1/2, anajifunza mtaala wa Mwaka wa 2 (Hatua ya 1), kama mwanafunzi wa Mwaka wa 4 katika darasa la 4/5/6 anavyojifunza mtaala wa Mwaka wa 4 (Hatua ya 2).

Kwa nini shule ya mtoto wangu ina madarasa ya miaka tofauti?

Madarasa ya miaka tofauti ni ya kawaida katika shule za Australia na yanaweza kuundwa kwa sababu ya:

- **Mifumo ya kujiandikisha** – ukubwa wa makundi ya mwaka hubadilika mwaka hadi mwaka. Madarasa ya miaka tofauti husaidia shule kuunda ukubwa wa madarasa ulio sawa.
- **Faida za kielimu** – shule zinaweza kutumia miundo hii ya darasa kwa sababu ya manufaa ya kujifunza na ya kijamii inayoweza kutoa.
- **Shule ndogo** – madarasa ya miaka tofauti ni kawaida katika shule ndogo na za vijijini, ambapo husaidia yanapounda madarasa kamili.

CC BY

Je, wanafunzi huwekwaje katika darasa la miaka tofauti?

Wakuu wa shule na walimu wanaamua nafasi za madarasa kwa kuzingatia:

- Ujifunzaji na ushiriki wa wanafunzi.
- Mchanganyiko wa wanafunzi kote shuleni.
- Usawa wa nguvu, mambo yanayovutia na mahitaji ya kujifunza.
- Ustawi wa kijamii na urafiki.
- Ufundishaji mzuri wa mtaala
- Mpangilio wa marekebisho na usaidizi katika madarasa yote.

Uwekaji wa madarasa hufanywa kwa maslahi ya wanafunzi ili kusaidia ujifunzaji. Kuwekwa katika darasa la miaka tofauti **hakumaanisha** kuwa mwanafunzi yupo juu au chini matarajio ya hatua za mtaala.

Je, kujifunza kunaonekanaje katika madarasa ya miaka tofauti?

Walimu hupanga ujifunzaji kwa kutumia mtaala wa NSW na hurekebisha ufundishaji wao ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi. Hii inaitwa **utofautishaji (differentiation)** na hutokea katika vyumba vyote vya madarasa kwa sababu wanafunzi hujifunza kwa viwango tofauti.

Katika darasa la miaka tofauti, walimu wanatumia mbinu mbalimbali za kuwasaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao. Hii inaweza kujumuisha:

- kufundisha darasa zima pamoja kwa baadhi ya shughuli
- kufanya kazi katika vikundi vidogo juu ya shughuli maalum za kujifunza
- kutofautisha kujifunza ili kutoa changamoto au usaidizi
- kurekebisha shughuli, rasilimali au njia ambazo wanafunzi wanaonyesha kujifunza kwao.

Maswali yako yamejibiwa

Je, mtoto wangu atapata umakini mdogo kutoka mwalimu yule?

Muundo wa darasa hauamui ni kiasi gani cha umakini mwanafunzi anachopokea. Walimu hupanga masomo wakijua wanafunzi wako katika hatua tofauti za kujifunza, kama vile vile katika madarasa ya mwaka mmoja.

Je, mtoto wangu atarudia kazi ambayo ameshafanya tayari?

Walimu hufuatilia maendeleo ya wanafunzi na hupanga masomo yao ipasavyo. Wanafunzi wataendelea kujifunza kutoka mtaala wao husika na wataungwa mkono kuendelea kujifunza mambo mapya.

Je, mtoto wangu atawaona marafiki zake bado?

Shule zinafikiria urafiki wakati wa kuunda madarasa. Wanafunzi pia wanaweza kuingiliana na marafiki zao wakati wa mapumziko na shughuli za shule nzima.

Je, madarasa ya miaka tofauti yataathiri mtoto wangu anavyofundishwa?

Walimu hutumia mafundisho dhahiri na warekebishe maelekezo kutegemea ujifunzaji, tathmini, nguvu na mahitaji. Hii inatokea katika kila aina ya darasa.

Je, mtoto wangu atakuwa na fursa za kuboresha au changamoto inayofaa?

Shule zote za umma za NSW husaidia wanafunzi wenye uwezekano mkubwa au uwezo wa kipawa chini ya Sera ya idara ya Elimu Yenye Uwezo Mkubwa na Kipawa. Walimu wanaangalia nguvu za wanafunzi na hupanga uboreshaji au upanuzi unaofaa ili ulingane. Hii inatokea katika kila aina ya darasa. Kuwekwa katika darasa la miaka tofauti hakuzuii fursa hizi.

Je, wanafunzi wenye ulemavu wanasaidiwa jinsi gani katika darasa la miaka tofauti?

Wanafunzi wenye ulemavu wanasaidiwa kushiriki kikamilifu katika kila darasa, ikiwa ni pamoja na madarasa ya miaka tofauti, kama ni katika mpangilio wa darasa kuu au la usaidizi. Walimu wanajifunza kujua uwezo, mahitaji na malengo ya kila mwanafunzi, na kutumia ufundishaji tofauti, marekebisho yanayofaa na, inapohitajika, mpango wa kibinafsi wa kujifunza na usaidizi ili kumsaidia kufanikiwa. Maamuzi hayo yanafanywa pamoja na wanafunzi inapofaa, na wazazi na wafanyakazi husika wa shule. Kuwekwa katika darasa la miaka tofauti hakubadilika mipango ya kibinafsi ya usaidizi.

Je, utafiti unasemaje?

Ufundishaji wa ubora wa juu ni ushawishi mkubwa shuleni kwenye ujifunzaji wa wanafunzi, kuwa na athari kubwa kuliko ukubwa wa darasa, muundo, au rasilimali nyingine. Utafiti unaonyesha kwamba wanafunzi katika madarasa ya miaka tofauti wanafikia matokeo sawa ya kitaalamu kama wanafunzi katika madarasa ya mwaka mmoja ambapo ufundishaji umepangwa vizuri na wanafunzi wanapokea usaidizi unaofaa. Madarasa ya miaka tofauti yanaweza pia kusaidia wanafunzi kukuza ushirikiano, huruma na mahusiano chanya na wenzao wa rika wa umri na uwezo mbalimbali.

Huduma ya mkalimani wa simu

Ikiwa utataka maelezo zaidi, tafadhali piga simu kwa mkuu wa shule. Ikiwa unahitaji mkalimani kukusaidia katika maulizo yako, tafadhali piga simu kwa Huduma ya Mkalimani wa Simu kwa 131 450 na omba kupata mkalimani katika lugha yako. Mwambie opereta wa simu nambari ile ya simu unayotaka kupiga na opereta wa simu atapata mkalimani kwenye simu ili kukusaidia na mazungumzo. Hutatozwa kwa huduma hii.